

# Kutumia mashine ya kudhibiti kiwango cha oksijeni kwa ajili ya msaada wa uamuzi wa COVID-19

Ilisashwa: 9 Aprili 2020, v1

## Mgonjwa ana dalili zozote zifuatazo?

- Homa (>38°C) kati ya siku 14 zilizopita
- Kukohoa au shida ya kupumua
- Kiwango cha kupumua kuongezeka
  - ≥22 kwa watu wazima (umri wa miaka 16 au zaidi)
  - ≥30 kwa watoto (umri wa miaka 5-15)
  - ≥40 kwa watoto wadogo (umri wa miaka 1-5)
  - ≥50 kwa watoto wachanga (miezi 2-11)
  - ≥60 kwa watoto chini cha miezi 2
- Ishara za dharura: kizuizi/kipingamizi cha kupumua; kushindwa kupumua kabisa; utoaji wa ngozi ya bluu; mshtuko; kuzimia; mtukutiko wa maungu.

**NDIYO**

## Angalia kiwango cha oksijeni kwa kutumia mashine ya kudhibiti kiwango cha oksijeni.

- Ikiwa kuna ishara za dharura, weka oksijeni mara moja.

**SpO2 < 94% AU  
Ishara za Dharura**

## Toa oksijeni ya ziada kupitia bomba la pua. Anzisha L/dak 5 (watu wazima) au L/dak 1-2 (watoto), dhibiti viwango vya mtiririko ili kudumisha SpO2 ≥ 90%.

- Angalia tena SpO2 baada ya dakika 15.
- Ikiwa kuna ishara za dharura, angalia tena ishara muhimu/SpO2 baada ya kila dakika 2-5, dhibiti viwango vya mtiririko ili kudumisha SpO2 ≥ 94%.

**SpO2 ≤ 90% AU  
Ishara za Dharura**

## Ongeza oksijeni ili kuongeza usaidizi wa mtiririko wa chini.

- Ikiwa inapatikana, tumia barakoa ya uso yenye kihifadhi (watu wazima) au kifuniko cha kichwa (watoto wachanga).
- Angalia tena SpO2 baada ya dakika 15.
- Ikiwa kuna ishara za dharura, angalia tena ishara muhimu/SpO2 baada ya kila dakika 2-5, dhibiti viwango vya mtiririko ili kudumisha SpO2 ≥ 94%.

**SpO2 ≤ 90% AU  
Ishara za Dharura**

## Laza kwa chumba cha wagonjwa mahututi, ikiwa kinapatikana.

- Ongeza usaidizi wa oksijeni na zingatia kuongezea msaada wa kupumua ikiwa unapatikana.
- Fuatilia SpO2 mtawalia, ikiwezekana.
- Ikiwa kuna ishara za dharura, kuwa na lengo la SpO2 ≥ 94%.

**HAPANA**

## Tathmini na usimamizi kwa kutumia itifaki za WHO/za ndani, pamoja na upimaji na kutengwa kwa ajili ya COVID-19 ikiwa imeashiriwa.

- Ikiwa mgonjwa anaonyesha hali ya kupumua kwa haraka, ugumu wa kupumua, shida ya kupumua, au ishara za dharura, tathmini tena mtiririko wa oksijeni kwa kutumia mashine ya kudhibiti kiwango cha oksijeni.

**SpO2 ≥ 94% bila Ishara za Dharura**

**SpO2 < 94% AU  
Ishara za Dharura**

**SpO2 ≥ 90% bila Ishara za Dharura**

## Endelea na usimamizi wa mgonjwa kwa kutumia itifaki za WHO/serikali.

- Angalia ishara muhimu/SpO2 baada ya kila saa 4-6 akiwa kwenye oksijeni.
- Dumisha SpO2 kati ya asilimia 90-96, kwa kupunguza kiwango cha mtiririko wa oksijeni inapowezekana.
- Kwa wagonjwa wajawazito, dumisha SpO2 kati ya asilimia 92-96.

**SpO2 ≥ 90% bila Ishara za Dharura**

**SpO2 ≤ 90% AU  
Ishara za Dharura**



# Ufafanuzi wa WHO wa COVID-19

**Mgonjwa aliye na ugonjwa kali wa kupumua (homa na angalau ishara moja au dalili ya ugonjwa wa kupumua, k.m. kukohoa, shida ya kupumua), NA historia ya kusafiri au kuwa na makazi katika eneo linaloripoti maambukizo ya ugonjwa wa COVID-19 katika kipindi cha siku 14, kabla ya dalili kuonekana;**

**AU**

**Mgonjwa aliye na ugonjwa wowote wa kupumua na ametangamana na mtu aliyethibitishwa au anayewezezana kuwa na COVID-19 katika siku 14 zilizopita kabla ya dalili kuonekana;**

**AU**

**Mgonjwa aliye na ugonjwa kali wa kupumua (homa na angalau ishara/dalili moja ya ugonjwa wa kupumua, k.m kukohoa, shida ya kupumua; NA anahitaji kulazwa hospitalini) NA kutokuwepo kwa utambuzi mbadala unaoelezea kabisa dalili za ugonjwa.**



Kwa maoni au maswali tuma barua pepe kwa: [covid@lifebox.org](mailto:covid@lifebox.org)  
[www.lifebox.org](http://www.lifebox.org)

